## 4.MAENEO TUNAYOTOA HUDUMA

Shirika la Viwango Tanzania (TBS), linatoa huduma zake kwa wadau wote wanaofanya vipimo vya kiutafiti, vya kisayansi na vya viwandani. Wadau hao ni Pamoja na

I.Mamlaka za Udhibiti
II.Maabara za upimaji
III.Viwandani
IV.Miradi ya ujenzi
V.Taasisi za elimu ya juu
VI.Hospitali

## 5.UHUSIANO WA KIMATAIFA

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kupitia sehemu yake ya Metrolojia ni mwanachama wa taasisi za kimataifa za vipimo za

I.International Bureau of Weights and Measures (BIPM)
II.Intra-Africa Metrology System (AFRIMETS)
III.Southern African Development Community Cooperation in Measurement Traceability (SADCMET)
IV.East African Metrology Technical Subcommittee (EAMET)

## 6.JINSI YA KUPATA HUDUMA

Huduma za metrolojia za Shirika la Viwango Tanzania (TBS), zinapatikana katika ofisi zake nne ambazo ni

I.Makao Makuu, Ubungo Dar es salaam
II.Ofisi ya Kanda ya Dar es Salaam
III.Ofisi ya Kanda Mashariki wa Ziwa, Mwanza
IV.Ofisi ya Kanda Nyanda za Juu Kusini, Mbeya

Utaribu wa kupata huduma za metrolojia

I.Tuma maombi ya kupatiwa huduma za ugezi kwenda kwenye email metrology@tbs.go.tz au kupitia namba ya simu 0733 700 440, au kupitia moja kwa moja kwenye mfumo wa shirika wa iSQMT.
II.Kufanya malipo: Mteja atapatiwa gharama za huduma Pamoja na ya malipo ya selikali (Control Number)
III.Huduma za metrolojia zitatolewa baada ya kupokea malipo
IV.Baada ya kufanyika kwa zoezi la ugezi, mteja atapata cheti cha ugezi (Calibration Certificate) kwenye mfumo.



TANZANIA BUREAU OF STANDARDS

tbs

www.tbs.go.tz
info@tbs.go.tz
metrology@tbs.go.tz
0800110827
+255 733 700 440

SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS)

TANZANIA BUREAU OF STANDARDS

tbs

# SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS)













# SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS)

## 1.UTANGULIZI.

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ni shirika la umma lililo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ambalo linatekeleza majukumu yake kama yalivyoanishwa katika Sheria ya Viwango, Sura 130. Moja ya majukumu hayo ni kutoa huduma za metrolojia.

Metrolojia ni sayansi ya vipimo inayohakikisha vipimo vinafanyika kwa usahihi na vinaaminika. Inajumuisha mbinu, vifaa, viwango, na taratibu zinazotumika kupima vitu mbalimbali.

## 2.HUDUMA ZA METROLOJIA

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linatoa huduma za Metrolojia ya Kisayansi na Metrolojia ya Viwandani. Metrolojia ya kisayansi ni tawi kuu la sayansi ya vipimo linalohusika na kutafiti, kutengeneza, Kunasibisha na kuendeleza vizio (units) na viwango (Standards) vya upimaji. Metrolojia ya Viwandani inahusisha matumizi ya sayansi ya vipimo katika uzalishaji na utoaji huduma, ili kuhakikisha vifaa vya kupimia vimefanyiwa ugezi (calibrated), vinapima kwa usahihi, na vinakidhi madhumuni.

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linatoa huduma za

I.Ugezi wa vifaa vya kupimia (Calibration)
II.Ushari wa kitaalamu kuhusu vipimo
III.Ulinganifu wa vipimo (Inter Laboratory Comparison)
IV.Kutunza viwango vya kitaifa vya upimaji (custodian of National Measurement standard)

## 3.MAABARA ZA UGEZI

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lina maabara sita za kutoa huduma za ugezi. Maabara hizo ni

I.Tungamo na Ujazo (Mass and Volume)
II.Umeme, Muda na Masafa (Electrical, Time and Frequency)
III.Themometria (Themometry)
IV.Urefu (Length)
V.Mekanikia (Mechanical)
VI.Kemikali na Biolojia: (Chemical and Biology)

Maabara hizi kwa Pamoja zinatoa huduma katika maeneo ya

I.Tungamo
II.Ujazo Mkubwa na mdogo
III.Umeme DC na AC
IV.Muda
V.Masafa
VI.Jotoridi
VII.Unyevu
VIII.Urefu
IX.Pembe
X.Mgandamizo (Pressure)
XI.Kani (Force)
XII.Toki (Tourque)
XIII.Kemikali
XIV.Biolojia
XV.Unyevu
XVI.Kemikali & Biolojia

Maabara za Shirika la Viwango Tanzania (TBS) zina cheti cha ithibati (Acreditation) kutoka taasisi ya Ithibati ya Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADCAS).



SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS)